



Atakayefunga Ramadhanani kwa imani na kutaraji malipo toka kwa Allah, atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia

Imepokewa Kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema:
Amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-: "Atakayefunga Ramadhanani kwa imani na kutaraji malipo toka kwa Allah, atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia"
[صحيح] [متفق عليه]

Anaeleza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa atakayefunga mwezi wa Ramadhanani kwa kumuamini Mwenyezi Mungu, na kwa kuitakidi ulazima wa swaumu na yale aliyoyaahidi Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa wafungaji kuwa na malipo makubwa na thawabu, akikusudia kupata radhi za Allah Mtukufu si kwa kutaka kujionyesha au kusikika, yatasamehewa kwake madhambi yake yaliyopita.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/4196>

